



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**  
**HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA**



**TAARIFA KWA UMMA**

**BARAZA LA MADIWANI LAPITISHA BAJETI YA SHILINGI BILIONI 84.30**  
**YA MWAKA WA FEDHA 2025/2026**

Mkutano wa baraza la madiwani la halmashauri ya manispaa ya Ilemela umepitisha rasimu ya mpango na bajeti ya **Tshs. 84,308,093,107.43** inayotarajiwa kutekelezwa katika mwaka wa fedha **2025/2026** ambayo ni sawa na ongezeko la **asilimia 9** ya bajeti ya mwaka wa fedha 2024/2025.

Kati ya fedha hizo **Tshs 9,569,975,546.00** ni ruzuku ya miradi maendeleo kutoka serikali kuu, **Tshs 55,293,406,450** ni fedha kwa ajili ya malipo ya mshahara ya watumishi, na **Tshs. 4,362,902,917** ni fedha za matumizi ya kawaida (OC).

Kwa upande wa mapato ya ndani manispaa ya Ilemela inatarajia kukusanya kiasi cha **Tshs. 15,081,808,193.95 (Shilingi Bilioni 15.08)** kutoka katika vyanzo vya mapato ya ndani ya halmashauri ikiwa imeongezeka kwa **asilimia 1.38** ukilinganisha na makisio ya mwaka 2024/2025 ambayo ni **Tshs. 14,876,400,000.00**.

---

Mkurugenzi wa Manispaa ya Ilemela, S.L.P 735, Mwanza.

Simu Na. +255(28) 2981196, Nukushi:+255(28) 2981196, BaruaPepe:md@ilemelamc.go.tz,

Tovuti: [www.ilemelamc.go.tz](http://www.ilemelamc.go.tz)

Aidha katika mwaka wa fedha 2025/2026, kiasi cha **Tsh. 6,544,354,376.00** kinakisiwa kutumika katika miradi ya maendeleo kutoka katika fedha za mapato ya ndani ya halmashauri.

Miradi ya maendeleo iliyopendekezwa kutekelezwa katika mwaka 2025/2026 itagusa sekta za **utawala, afya, elimu, Barabara, maendeleo ya jamii, uvuvi, fedha na biashara, TEHAMA, mazingira, mipangomiji, mipango, takwimu na ufuatiliaji sambamba na udhibiti wa taka.**

Mapendekezo ya rasimu ya mpango na bajeti ya halmashauri yamewasilishwa na mchumi wa manispaa ya Ilemela, ndugu Herbert Bilia ambae amesema kuwa mapendekezo haya yameandaliwa kwa kuzingatia sheria ya bajeti namba 11 ya mwaka 2015.



Violencea S. Mbakile  
Mkuu Kitengo cha Mawasiliano Serikalini  
**30 JANUARI, 2025**